

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Telagrams: **"REGCOM COAST"**  
Tel. No. 023-2402287/2402066  
Fax No. 023-2402358/2402151  
E- Mail: [ras@pwani.go.tz](mailto:ras@pwani.go.tz)  
[ras.pwani@pmoralg.go.tz](mailto:ras.pwani@pmoralg.go.tz)



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
Mkoa wa Pwani,  
S. L. P 30080,  
**KIBAHA.**

**TAARIFA KWA UMMA.**

**UFANYIKAJI WA MTIHANI WA TAIFA WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2018**

Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi kwa mwaka 2018 umeanza kufanyika tarehe 5 na 6/09/2018. Mtihani huo utahusisha masomo ya Kiswahili, Kiingereza, Maarifa ya jamii, Hisabati na Sayansi.

Mkoa wa Pwani una jumla ya Halmashauri tisa zenye shule za Msingi 575. Kati ya shule hizo, Shule 533 zinatumia mfumo wa Kiswahili na shule 42 zinatumia mfumo wa Kiingereza.

Jumla ya watahiniwa 30,115 wamesajiliwa kufanya mtihani huo ambapo watahiniwa 28,827 wakiwemo wavulana 13,726 na wasichana 15,101 wameisajiliwa katika shule zinazotumia mfumo wa Kiswahili na watahiniwa 1,288 wakiwemo wavulana 635 na wasichana 653 wamesajiliwa katika shule zinazotumia mfumo wa Kiingereza.

Miongoni mwa watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani huo, wapo watahiniwa 54 wenye uoni hafifu. Watahiniwa 51 wakiwemo wavulana 26 na wasichana 25 wamesajiliwa katika shule zenye mfumo wa Kiswahili na watahiniwa 3 wote wavulana wamesajiliwa katika shule zenye mfumo wa Kiingereza.

Jumla ya mikondo 1,430 ilitumika katika kuwatahini wanafunzi hao. Mikondo 1,331 imetumika kutahini watahiniwa wanaotumia mfumo wa Kiswahili, pamoja mikondo 32 ya watahiniwa wenye uoni hafifu. Aidha mikondo 65 itatumika kutahini wanafunzi wanaotumia mfumo wa Kiingereza, pamoja na mikondo 2 ya wanafunzi wenye uoni hafifu.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhe. Mhandisi Evarist Ndikilo anawatakia wanafunzi wote mtihani mwema, kuwa watulivu kwa kuzingatia sheria na taratinu za Mitihani.

Imetolewa na :

Nasra Mondwe  
**AFISA HABARI**  
**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**PWANI**  
5 Septemba, 2018